

## Mwanzo 2:5-6

*[5]hapakuwa na mche wa kondeni bado, wala mboga ya kondeni haijachipuka bado, kwa maana BWANA Mungu hajainyeshea nchi mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi;*

*[6]Jukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji juu ya uso wote wa ardhi.*

Tofauti na inavyodhaniwa, kwamba mvua ilinyesha juu ya nchi siku ile Mungu alipozichepusha mbegu ardhini. lakini haikuwa hivyo. Japokuwa hilo liliwezekana. Lakini Mungu hakutumia njia hiyo

kinyume chake alileta ukungu, ambao ni unyenyevu juu ya ardhi yote kutoka chini. Ukailowesha ardhi yote. Na hivyo mbegu zikapata uhai, zikamea.

Tunaona jambo kama hili alilifanya tena..wakati ule wa wafalme pindi walipotoka kwenda kupigana na wamoabu waliowaasi, biblia inatuambia walizunguka siku saba, bila maji, hatimaye wakamuuliza Bwana wafanyeje.

Ndipo Bwana akawaambia..chimbeni mahandaki, kisha nitayajaza maji bila mvua

## 2 Wafalme 3:16-18

*[16]Akasema, BWANA asema hivi, Fanyeni bonde hili lijae mahandaki.*

*[17]Kwa kuwa BWANA asema hivi, Hamutauona upepo, wala hamtaiona mvua, ila bonde hilo litajaa maji; nanyi mtakunywa, ninyi, na ng'ombe zenu, na wanyama wenu.*

*[18]Na jambo hili ni jepesi machoni pa BWANA; pia atawatia Wamoabi mikononi mwenu.*

## Ni Kutufundisha Nini?

Bwana hushibisha kutoka juu, lakini pia hushibisha kutoka chini. Utakufunulia mambo yake ya rohoni moja kwa moja kutoka mbinguni,

lakini pia atakufunulia kutoka hapa hapa duniani kupitia mambo yanayokuzungua yaani watu, vitu, n.k. na vyote vikaleta matokeo yale yale. Atakupa mahitaji yako kimiujiza, lakini pia kwa kupitia watu. Mungu wa vilivyo juu ndio Mungu yule yule wa vilivyo chini.

Ndivyo anavyotenda kazi, ili tusimzoelee uweza wake.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

**Mafundisho mengine:**

Tafsiri ya Mwanzo 2:6 Ukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji.

*HUIJUI KAZI YA MUNGU, AFANYAYE MAMBO YOTE.*

*NUHU WA SASA.*

*Biblia inaposema Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana, Inamaana gani?*

## **Rudi Nyumbani**

Share on:  
WhatsApp